**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA TISA

**07 FEBRUARI, 2020**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 07 FEBRUARI, 2020

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Azimio la kufuta Hasara itokanayo na Maduhuli ya Madeni ya Nyuma ya Ada na Leseni za Magari, Riba na Adhabu kwa Kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2019.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (Mapitio ya Nusu Mwaka 2019/2020) *[Monetary Policy Statement (The Mid-Year Review 2019/2020)].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Azimio la kufuta Hasara itokanayo na Maduhuli ya Madeni ya Nyuma ya Ada na Leseni za Magari, Riba na Adhabu kwa Kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2019.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la kufuta Hasara itokanayo na Maduhuli ya Madeni ya Nyuma ya Ada na Leseni za Magari, Riba na Adhabu kwa Kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2019.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 *(The Arbitration Bill, 2020).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 *(The Arbitration Bill, 2020).*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 *(The Arbitration Bill, 2020).*

## III. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

### 105. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wakati akiwaapisha Wakuu wa Mikoa tarehe 15 Machi, 2016 Mhe. Rais alitoa agizo la kuwakamata Vijana wote watakaokutwa wakicheza mchezo wa *“pool table”* na kupelekwa kambini wakalime:-

(a) Je, Serikali imeandaa kambi ngapi na kujua huduma za kujikimu kwa Vijana hao wakati watakapokuwa wakiendelea na shughuli za kilimo na kipindi cha kusubiri mavuno yao;

(b) Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kupunguza tatizo la ajira kwa Vijana ili kuondokana na wimbi la Vijana kuzurura na kushinda bila kufanya kazi;

(c) Je, Serikali imefanya sensa na kujua ni Vijana wangapi wanaofanya kazi usiku na kupumzika mchana au mchana na kupumzika usiku ili kubaini wazururaji wa mchana na wanaocheza *“pool table”* mchana kwa sababu ya kukosa ajira.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 106. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuangalia Bajeti ya Hospitali ya Wilaya ya Urambo ambayo inahudumia Wananchi wa maeneo ya Kaliua, Ulyankulu na maeneo ya jirani ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma;

(b) Hospitali ya Wilaya ya Urambo ina majengo mawili ya *ICU* na Maabara ambayo hayajakamilika tangu yalipoanza kujengwa 2011 kupitia utaratibu wa *LODG* ya mradi wa *ADB*; Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu ombi la Wananchi wa Urambo la shilingi milioni mia mbili ambazo zinaweza kumaliza majengo hayo;

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kuongeza Wafanyakazi angalau Manesi 12 na Wafamasia 6 kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Wagonjwa Hospitalini hapo.

**107. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kati ya Kijiji cha Mbori na Kijiji cha Tambi upo Mto ambao hujaa maji wakati wa mvua na kusababisha Wananchi na baadhi ya Wanafunzi wa Shule ya Msingi Tambi na Sekondari ya Matomondo kushindwa kuvuka kwenda Shule:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja katika Mto huo ili Wananchi na Wanafunzi waweze kuvuka.

**108. MHESHIMIWA ENG. EDWIN AMANDUS NGONYANI (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Vijiji vinavyounda Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori waliopo Namtumbo miaka 14 iliyopita walikubaliana kuacha ardhi yao kwa shughuli za hifadhi na kwamba ardhi hiyo isitumike kwa makazi wala kilimo cha mazao ya kudumu isipokuwa Mpunga pekee. Wananchi washiriki kutunza njia za asili za wanyama hususan Tembo na mipaka ya ardhi husika ingepitiwa upya baada ya kupita miaka 10 kuanzia mwaka 1996 walipoingia makubaliano:-

(a) Je, kwa nini Serikali imekiuka makubaliano hayo na kuwakaribisha Wafugaji kwenye maeneo ya Wananchi yaliyokuwa yakitumika kwa kilimo cha Mpunga;

(b) Je, ni lini Serikali italipa fidia Wakulima ambao mashamba yao ya Mpunga yameathiriwa na Ng'ombe wanaochunga katika mashamba hayo.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**109. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Wavuvi wa Kisiwa cha Ukerewe hawana elimu wala mitaji ya kutosha:-

Je, ni Vikundi au Wavuvi wangapi katika Kisiwa cha Ukerewe wamepewa elimu na mitaji ili waweze kufanya uvuvi wenye tija.

**110. MHESHIMIWA HAMADI SALIM MAALIM (KOJANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Uvuvi si suala la Muungano, na Wavuvi wengi wa Visiwa vya Unguja na Pemba wanapokuwa katika maeneo mbalimbali ya mwambao wa Afrika Mashariki hukumbana na changomoto nyingi ikiwemo

kukamatwa wanapokuwa katika shughuli zao za uvuvi, kutozwa tozo zisizo za lazima nk:-

Je, Serikali imejipangia mikakati gani ili kupunguza changamoto hizo.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**111. MHESHIMIWA SALUM MWINYI REHANI (UZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

(a) Je, ni lini Mamlaka ya Hali ya Hewa itakuwa inatoa taarifa sahihi na za wakati kuhusiana na mabadiliko ya hali ya hewa nchini;

(b) Je, ni lini Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na Idara ya *Earthy Warming* watakuwa wanatoa taarifa za hali ya upatikanaji wa mvua na ukame ili kuwaepusha Wakulima wengi kulima na kupata hasara kwa kukosa mvua wakati wao wanajua hali itakavyokuwa.

**112. MHESHIMIWA HASSAN ELIAS MASALA (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini barabara ya Masasi – Nachingwea – Nanganga itajengwa kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**113. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Utalii wa Uwindaji, Utalii wa Picha na ufugaji wa Mapori na Misitu ya Hifadhi ya Ugunda, Isuvangala na Ipembampazi ni miongoni mwa fursa kuu za utalii kwenye Jimbo la Sikonge:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege uliokuwa umeanza kujengwa karibu na mlima wa Ipole ambao ulijumuisha pia ujenzi wa nyumba za kufikia Watalii *(Tourist Rest House)* kwenye Kijiji cha Ugunda.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**114. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Elimu ya Msingi ni muhimu kuwawezesha Wahitimu kuzalisha na kuwapa stadi za maisha. Lakini wapo Wahitimu wa Elimu ya Msingi, Sekondari na

Vyuo wasioweza hata kuanzisha bustani za mboga mboga na matunda:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha elimu inayotolewa inamuwezesha Mhitimu kupata ujuzi na stadi za maisha ili aweze kujiajiri.

**115. MHESHIMIWA ASHA ABDULLA JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Wapo Watoto wengi wenye uwezo (ubongo) mzito wa kufahamu kusoma au kuandika na hatimaye kubakia shule kwa muda mrefu:-

Je, Serikali ina mkakati gani juu ya kundi hili kubwa la Watoto katika kuwaendeleza kielimu ili kuweza kujitegemea.

**WIZARA YA MAJI:**

**116. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani kwa sasa wa kutatua kero ya maji katika Jimbo la Momba.

**WIZARA YA KILIMO:**

**117. MHESHIMIWA JOSEPH KIZITO MHAGAMA (MADABA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-
Miongoni mwa mambo yanayokwamisha ukuaji wa sekta ya Kilimo nchini ni pamoja na kukosekana kwa maduka ya pembejeo za kutosha maeneo ya Vijijini ambako ndiko walipo Wakulima wengi. Miongoni mwa sababu za kukosekana maduka hayo ni gharama kubwa ya kufuzu *(certifications)* kama vile TOSC 1 Tsh. 100,000/=, TPRI Tsh. 320,000/=, TFDA Tsh. 100,000/=, leseni n.k. na hivyo kufanya gharama ya zaidi ya Tsh. 600,000/=:-

Je, ni kwa nini Serikali isiondoe gharama hizo ili kutoa hamasa kwa Wajasiriamali kupata mafunzo, kufuzu na kuwekeza maduka ya pembejeo ili kusogeza huduma kwa Wakulima wadogo na kuharakisha kasi ya ukuaji wa Kilimo.

**118. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni vigezo vipi vinatumika kumpata Mwenyekiti wa Bodi ya Ushirika.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2020 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2020].*

Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea wa Mwaka 2020 *(The Plant Health Bill, 2020).*

Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa Mwaka 2020 *(The Deep Sea Fisheries Management and Development Bill, 2020).*

## V. HOJA ZA SERIKALI:

**AZIMIO:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Azimio la kufuta Hasara itokanayo na Maduhuli ya Madeni ya Nyuma ya Ada na Leseni za Magari, Riba na Adhabu kwa Kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2019.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 *(The Arbitration Bill, 2020).*

## VII. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

## VIII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

**WAZIRI MKUU.**

## IX. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

**DODOMA**
**07 FEBRUARI, 2020**

**S. KAGAIGAI**
**KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA